2. **Kusoma**

**Shughuli ya 1 ufahanu wa kifungu cha simulizi uk 37- 39.**

**1**( a) Tunasoma ufahamu ili :

(i) kupata maarifa mapya.

(ii) Kukuza uwezo wa kufukiri

( iii)Kujenga na kukuza mbinu za kuandika

( iv) Kunoa uwezo wa mawasiliano .

( v) Kukuza msamiati na stadi za lugha .

( v) Kupata burudani

( vi ) Kuchochea na kukuza ubunifu .

b) Mambo yanayosaidia kuelewa vifungu vya ufahamu .

(i) Kuwa makini unaposoma kifungu cha ufahamu.
(ii)Kujaribu kukizia maana ya msamiati kulingana na muktadha .
(iii) Kujiuliza maswali ya kujitathmini kama vile kifungu hiki kinahusu nini ? Nimejifunza nini ?
(iv) Kusimulia kifungu kwa wengine .
( v) Kutafuta maana ya msamiati kwa kamusi .

2. Soma kifungu kwa kuzingatia mbinu za usomaji bora wa vifungu vya ufahamu .

3. ( i) Lugha iliyotumika katika kifungu ni ya kawaida inayoeleweka kwa urahisi .

( ii ) Matukio katika kifungu hiki yanafuatana moja kwa moja kwa mtindo sahili kuanzia mwanzo hadi mwisho .

( iii) Matukio ya ufahamu yanajitokeza kwa njia ya masimulizi .
( iv ) Vitendo vya safina vinajenga matukio na kuelezwa kwa kina .

4.(a) - Alitandika kitanda chake kwa shuka safi .

- Aliweka shuka chafu kwenye kapu la nguo chafu .
- Alipiga meno mswaki na kunawa uso.

( b)( i) Kapu la nguo chafu (ii) taulo (iii) mswaki na dawa ya kupiga mswaki (iv) Sabuni ( v) Kitana ( vi ) Mafuta ya nywele ( vii) Vipodozi na sodo ( viii )Kabati (ix) Mashine ya kuosha nguo .

( c ) Safina alitumia vifaa vifuatavyo kudumisha usafi .
( i ) Maji ( ii) sabuni ( iii) mafuta ( iv) mswaki na dawa ya kupigaswaki(v)Vipodozi( vi) Kitana( Vii ) Sodo .

( d) Aina za usafi wa kibinafsi zilizotajwa katika kifungu ni pamoja na :
( i) Usafi wa mwili - safina alioga mwili wote na kutumia vipodozi . Pia alipiga meno mswaki . ( ii ) Usafi wa malazi

-anatumia shuka safi kutandika kitanda chake .

( iii) Usafi wa mazingira - anapanga chumba chake vizuri . Anapanga pia kabati vizuri.

( iv) Usafi wa mavazi - anaosha nguo na shuka chafu .

( v) Usafi wa vyakula - anaosha matunda kabla ya kuyala .

4. Matukio yanafuatana ifuatavyo

C, e , b, a , d .

5. ( a) Safina hangeweza kushughulikia usafi wa nyumbani kama vile kupanga chumba chake na kuosha nguo zake chafu.

( b ) Meno yake yangepoteza weupe wake na pia angenuka mdomo .

( c) Haingekuws rahisi kuziosha nywele na kuzichana.
( d) Haingekuwa rahisi kuziosha kwa mikono na ingemlazimu kutumia mashine .
( e) Kucha hizo zingehifadhi uchafu ambao hubeba viini ambavyo vingemsababishia magonjwa .

6. ( i ) Safi - isiyo na uchafu
( ii ) Taulo -kipande cha nguo maalum kinachotumiwa kufutia mwili baada ya kuoga
( iii) Sabuni - kitu kinachotoa povu kinapochanganywa na maji na ambacho hutumiwa kutekeleza usafi .

(iv ) Kuzichana - kuzitengeneza nywele kwa kutumia kitana .

( v ) Chawa - mdudu anayeletwa na uchafu na ambaye hukaa kwenye nywele au nguo chafu .

( vi ) Sodo - kifaa kinachotumiwa na wanawake kudumisha usafi wakati wa hedhi.

**Dijitika**
Shughuli ya a - d ikamilishwe kikamilifu .

**Nje ya darasa**

Shughuli ya a na b ikamilishwe .

Shughuli ya 2. Kusoma kwa mapana : Matini ya kujichagulia .

1 ( a) Matini mbalimbali kama vile matini ya kisayansi , burundani , kitaaluma zitajwe .

( b) Rejelea sehemu ya kumbuka uk 41- 42.

2. Msamiati wa lishe bora uliotumika katika matini ni pamoja na
( i ) Wanga ( ii ) virutubisho ( iii) protini ( iv ) vitamini ( v) mafuta ( vi ) kalori .

( b) ( i ) Wanga - chakula kinachompa mtu nguvu .

( ii) Virutubisho - viini vinavyopatikana katika chakula na ambavyo ni muhimu kwa ukuaji wa viumbe .

( iii) Protini - thamani katika chakula ambayo husaidia kujenga mwili.

( iv) Vitamini - virutubisho katika chakula ambavyo humpa mtu kinga dhidi ya magonjwa.

( v) Mafuta - kitu kama maji ambavyo hupatikana katika aina fulani za matunda na wanyama kama samaki.
( vi ) Kalori - vipimo vya virutubisho mbalimbali vinavyohitajika mwilini

( C) (i) Lishe - chakula chenye virutubisho vyote muhimu .
( ii ) virutubisho - viini katika chakula na ambavyo ni muhimu kwa ukuaji wa binadamu .

(iii) Kalori - vipimo vya virutubisho mbalimbali vinavyohitajika mwilini

( iv ) Kinga - uwezo wa mwili kupigana na magonjwa.

(v) Kisukari - ugonjwa ambao humpata mtu viwango vya sukari vikizidi au kupungua mwilini.

( vi ) Kudumaa - kutokua vizuri kwa binadamu kutokana na lishe isiyofaa .

( vi ) Saladi - matunda na mboga zilizokatwakatwa na kuliwa zikiwa bichi .

( d) Sentensi zionyeshe matumizi yanayofaa ya msamiati husika .

( e ) Lishe bora ni muhimu kwa ukuaji wa mwili na kuuwezesha mwili kupigana na magonjwa .

( f) Muhtasari ujumuishe hoja zifuatazo

( i ) Lishe bora hujumuisha chakula chenye virutubisho muhimu ambavyo ni muhimu kwa ukuaji na kukinga mwili dhidi ya magonjwa .

( ii ) Lishe bora husaidia ukuaji na ikikosekana madhara yake hujidhihirisha kwa njia mbalimbali kama vile magonjwa na kudumaa .

( iii) Lishe bora humsaidia binadamu kuwa na ngozi na nywele nzuri .

( iv) Ili kupata lishe bora chakula kiliwe bila kuraka mlo wowote , mara tatu kwa siku na kijumuishe matunda .

( v) Maji pia ni sehemu muhimu ya lishe bora .

( vi ) Vitu ambavyo vinasisimua mwili viepukwe .

( g ) Wasilisha uliyoyarekodi kwa wenzako .

**Dijitika**

Shughuli za a - f zikamilishwe .

**Nje ya darasa**

1. Matini ilenge lishe bora .
2. Matini isomewe mzazi au mlezi .
3. Sababu zijitokeze waziwazi .

**Shughuli ya 3 Kusoma kwa kina : Novela uk 42- 43.**

1. ( a) Novela - Ni kisa cha kubuni kinachoandikwa kwa lugha ya nathari chenye urefu wa wastani.

( b) ( i ) Yaliyomo au maudhui - maudhui ni mambo yanayozungumziwa katika novela . Katika novela maudhui huwa machache kuliko yale ya riwaya lakini mengi kuliko hadithi fupi .

( ii ) Urefu - Novela huwa na urefu wa wastani kati ya kurasa 96- 100 . Huwa ndefu kuliko hadithi fupi lakini fupi kuliko riwaya .

( iii ) Mtindo - hutumia mtindo usio changamano . Kwa mfano hakuna matumizi mengi ya mbinu rejeshi .
Kutakuwa na mbinu za kimtindo kama vile methali , nahau , misemo , chuku , tashihisi , taswira , kejeli , kinaya n.k

( v) Ploti - novela huwa na ploti sahili . Matukio hufuatana moja kwa moja bila matumizi ya mbinu rejeshi .

( vi ) Wahusika - wahusika huwa si wengi sana kama katika riwaya . Wahusika wakuu huwa wachache na mwadishi hana nafasi kubwa sana ya kuwakuza .

( vi ) Matukio - matukio ya novela huwa si mengi kama vile katika riwaya .

2. Sifa zinazoafiki novela ni
a , d, f na h

3. ( a) Urefu - urefu ni wa wastani .Huwa na kati ya kurasa 96- 100
( b ) Ploti - huwa na ploti sahili ambapo matukio hufuatana moja kwa moja bila matumizi ya mbinu rejeshi .

( c) Lugha - si changamano . Huwa sahili .

( d) Maudhui - maudhui huwa machache .

( e ) Mandhari - mandhari huwa si changamano .  Yanajitokeza waziwazi .

( f ) Wahusika - huwa wachache kuliko wale wa riwaya na huwa hawajakuzwa kikamilifu

4.Mwanafunzi baada ya kusoma novela atambue sifa kama vile:
( i ) Si ndefu sana
( ii ) Haina migawo ya sura
( iii ) Ploti huwa sahili
( iv ) Wahusika huwa wachache na wasiokuzwa kikamilifu .
( v)  Maudhui huwa machache .
( vi ) Mandhari huwa si changamano .

**Dijitika**

( a ) Maana na sifa za novela kama zilivyoelezwa katika swali la 3 na 4 sijitokeze .

( b) Sifa za novela zijitokeze kama zilivyo katika 3 na 4 hapo juu .

( c ) Wenzako waweze kutambua sifa za novela . Rejelea 3 na 4 hapo juu .

**Nje ya darasa**

Sifa za novela zijitokeze barabara .

**Shughuli ya 4. Kusoma kwa ufasaha**

1 ( a) Kusoma kwa ufasaha ni kusoma kwa kuzingatia vipengele vya usomaji bora. Hivi vipengele ni pamoja na utamkaji bora wa maneno , kuzingatia kasi inayofaa , sauti inayosikika na matumizi ya ishara zinazofaa .

( b ) Vipengele vya kuzingatia katika kusoma kifungu kwa ufasaha  vilingane na vile vilivyoorodheshwa katika sehemu ya *kumbuka* uk 44 .

2 a) Mwanafunzi asome kifungu kwa kuzingatia vipengele vya usomaji bora .

b) Maoni ya wanafunzi yajikite katika kumwelekeza mwenzao katika mbinu na vipengele vya usomaji bora .

**Dijitika**

a) Mwalimu aelekeze wanafunzi jinsi ya kupata makala yanayofaa .
b) Vipengele vya kusoma kwa ufasaha ambavyo vinaweza kuzingatiwa ni pamoja na.

i)  Utamkaji bora wa maneno
ii) Kuzingatia kazi inayofaa
iii) Kutumia sauti inayosikika vizuri

iv)Matumizi ya Ishara zinazofaa
v) Matumizi ya toni na kimbo kinachofaa .

C) wanafunzi wasomewe vipengele vilivyo hapo b ) juu .

**Shughuli ya 5 Kusoma kwa ufahamu : Kifungu cha ufahamu .**

1. Habari mahasusi zinazojitokeza katika kifungu hiki .

- Kuwa licha ya tofauti za kimaumbule zisizopingika kati ya wanaume na wanawake hakuna jinsia iliyo bora kuliko nyingine .
- Dhuluma kwa misingi ya jinsia haifai
- Kuwa bado zipo jamiii ambazo zinazingatia tamaduni zinazotenga majukumu katika jamii kwa misingi ya jinsia .
- Kuna ubaguzi wa kijinsia katika ajira ambapo watu hunyimwa kazi fulani kwa sababu ya jinsia zao.
- Usawa wa Kijinsia ni kigezo muhimu katika kuhakikisha ustawi wa nchi .
- Twafaa kupiga hatua kwa kupuuza mitazamo ya kale kuhusu jinsia .

b) **Ufupisho**

•Hatua za kuandika ufupisho kama zilivyoekezwa katika Uk 47- 48 zizingatiwe .
•Hoja zote muhimu zijumuishwe . Hizi ni pamoja na.
- Tofauti za kimaumbile kati ya mwanaume na mwanamke zi wazi na hasipingiki.
- Wanaume na wanawake wamepewa uwezo wa kutekeleza majukumu yoyote bila kujali jinsia .
- Ni dhuluma kuachia jinsia moja baadhi ya majukumu
- Zipo jamii ambazo zimetenga baadhi ya majukumu kwa jinsia fulani na kuona mwiko majukumu fulani kutekelezwa na jinsia fulani.
- Kuna ubaguzi katika ajira kwa misingi ya jinsia .
- Usawa wa kijinsia ni kigezo muhimu katika kuhakikisha usawa ustawi wa nchi .
- Ulimwengu wa sasa haufai kukubali ugawaji wa majukumu kwa misingi ya jinsia .

(C)
(i) Jinsia - hali ya kuwa mwanaume au mwanamke , uana
( ii ) Ubaguzi - unyimaji wa watu kazi kwa misingi ya kijinsia .
( iii ) Majukumu - wajibu wa mtu katika jamii. Mambo Yanayofaa kutekelezwa na mtu fulani

( iv) Ndwele - ugonjwa

2. a- f tekeleza shughuli zote .

*Nje ya darasa*
1. Tafuta kifungu mwafaka
2. ( a) Habari muhimu zindondolewe.
( b) Fupisha ujumbe kwa kuzingatia utaratibu bora wa ufupishaji

( c) Msomee mzazi au mlezi ufupisho wako
( d) Mweleze mlezi au mzazi maana ya msamiati kutoka kifungu hicho .

**Shughuli ya 6 uk 48**

1. Dhamira ni lengo la kazi fulani ya fasihi
2. a) Mwandishi alilenga kuonyesha matarajio ya wazazi kuhusu ya maendeleo ya watoto wao .
( b) Mwandishi analenga kuonyesha matarajio ya jamii kuhusu maendeleo ya watoto kupitia masomo na jinsi jamii ilivyoenzi masomo ya watoto wa jinsia zote .

Aidha , mwandishi anaendelea kuonyesha umuhimu wa wazazi katika kuwaelekeza watoto wao katika njia zitazofaa.

Mwandishi hata hivyo pia anaonekana kulenga pia kuonyesha kuwa Jitihada haiondoi kudura na liandikwalo ndilo liwalo kwani Zureya anakatiza masomo yake ghafla na kuamua kumfuata swahibu aliyeishi mashariki ya mbali kinyume na matarajio ya babake .

**II**

1. ( a) maudhui ni mambo yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi
(b) Shughuli itekelezwe

2 ( a) Maudhui mbalimbali yanajitokeza yakiwemo :
( i) Kilimo - mzee Makini alikuwa mkulima . Alikuwa amepanda aina mbalimbali za matunda na mboga na kuwafuga wanyama na ndege mbalimbali .
( ii ) Elimu - jamii hii ilithamini masomo ya mtoto msichana na tunaona Mzee Makini akifanya kila jitihada kumsomemesha mtoto wake Zureya .

( iii) Usawa wa jinsia katika masomo - Jamii alithamini masomo ya mtoto msichana .

( iv) Uwajibikaji - wazazi wanawajibika kutekeleza majukumu yao. Kwa mfano familia ya mzee makini inaonyesha uwajibikaji kwa kumsomesha mtoto wao Zureya .
( V) Malezi bora - Makini alimkumbusha bintiye kila siku umuhimu wa nidhamu katika maisha .

b) Muhtasari ulenge maudhui yaliyojadiliwa hapo juu .

**Shughuli Jumuishi ( a - f)**
Tekeleza shughuli zote .

**Nje ya darasa** ( 1-3)
Shughuli zote zitekelezwe .

**Shughuli ya 7 : Ufupisho Uk. 51**

1 ( a) ufupisho ni kueleza upya habari kwa maneno machache bila kupotosha ujumbe .

( b) Kifungu kina aya sita . Ujumbe katika kila aya unaweza kufupishwa ifuatavyo

1. Shule ya Huduma ilikuwa na furaha kupata nafasi ya kuwa mwenyeji wa Tamasha la muziki baada ya muda mrefu
2. Mwalimu mkuu aliandaa mkutano wa viranja katika ukumbi wa mikutano
3. Mwalimu mkuu Bi . Kerubo aliwaeleza viranja alichowaitia .
4. Wanafunzi wakiongozwa na viranja walifanya maandalizi kwa kuzingatia usafi shuleni kote .
5. Sehemu zote za shule ziling'arishwa
6. Kiranja mkuu aliwajibika vilivyo katika kuongoza maandalizi ya siku hiyo ambayo waliitarajia kwa hamu sana .

( C) Ufupisho ujumuishe hoja zote zilizoorodheshwa katika *b* hapo juu na zikiwa zimeunganishwa kujenga aya .
( d) Wasilisha ufupisho uliouandika kwa wenzako wautolee maoni.

2. ( a- b) Tafuta matini ya kidigitali , uisome na uifupishe kwa kuzingatia hatua za ufupishaji zilizoorodheshwa katika sehemu ya **kumbuka** hapo juu ( uk 52)

**Nje ya darasa** ( 1-4)

Shughuli zote zitekelezwe .

**Shughuli ya 8 Kusoma kwa kina : Mandhari na ploti**

1. Mandhari katika fasihi hurejelea sehemu au mazingira ambamo matukio yanatendeka.
Nayo ploti hurejelea jinsi matukio yalivyopangwa katika kazi ya fasihi . Ni mtiririko wa matukio katika kazi fulani ya fasihi.

2. Mambo yafuatayo huzingatiwa ili kutambua mandhari ya novela .

( i ) Maelezo ya mwandishi kuhusu mahali wanamoishi wahusika . Aina za majengo n.k
( ii) Maneno ya wahusika wenyewe kuhusu hali zao za kiuchumi , kijamii n.k.

( iii ) Kipindi / Muda - wahusika wanaishi katika kipindi gani cha kiwakati. Hili laweza kujitokeza kupitia maneno ya wahusika , maelezo ya mwandishi.

( iv ) Muktadha wa kiuchumi na kijamii wa jamii inayohusika . Je wahusika wanaishi maisha ya aina gani ?

( V) Hisia za wahusika - zingatia hisia za mwandishi kuhusu hali na maisha ya wahusika. Pia hisia za wahusika wenyewe kuhusu maisha yao wenyewe yanaweza kudokeza aina ya mandhari .

( Vi ) matendo ya wahusika . Matendo ya wahusika yanaweza elekeza msomaji kutambua mandhari . Kwa mfano ukiwa wahusika wanalala njaa jambo hilo linaweza kuelekeza msomaji kuhusiana na hali ya kiuchumi ya wahusika ...

( b) Tambua mandhari mbalimbali kama vile .

( i) Madhari ya kisiasa kama vile mifumo ya kisiasa , hali ya kisiasa katika jamii husika n.k
(ii) Mandhari ya kijamii kama vile hali ya masomo , miundo mbinu ya kijamii kama vile shule , hospitali n.k
( iii ) Mandhari ya kiwakati / kihistoria
( iv ) Mandhari ya kijiografia kama vile misitu , mito ,milima n.k

(C) Mandhari huwa na dhima ama umuhimu ufuatao katika fasihi;

( i) Husaidia kujenga na kukuza maudhui
( ii) Husaidia kuwasilisha dhamira na ujumbe
(iii) Huwezesha sifa za wahusika kujitokeza
(iv) Hukuza mivutano na migogoro katika hadithi
( v) Hukuza muktadha wa novela .

( d) (i) Kuuza na kununua kama vile katika mandhari ya mjini
( ii ) Shughuli kama vile kulima katika mandhari kama vile ya mashambani
( iii ) Shughuli za masomo katika mandhari ya shuleni na vyuo .
( iv ) Katika mandhari ya kiasili kama vile milima kutakuwa na shughuli kama vile kukwea milima n.k
(v) Katika mandhari ya kisiasa kutakuwa na mambo kama vile kampeni na upigaji kura ukiendelea .

( e) Madhari ufanikisha ujumbe kwa njia zifuatazo

( i ) Huleta uhalisia - kwa mfano uhalisia wa maudhui ya umaskini utaletwa na mandhari yenye makazi hafifu , watoto wanaovaa matambara n.k

( ii ) Hukuza hisia zilizokusudiwa na mwandishi .Kwa mfano hisia za huruma , za furaha ..

( iii ) Mandhari hufanikisha ujumbe kwa kutoa muktadha uliokusudiwa
( iv) Huchochea wasomaji Kushwaha hatua
( v) Husaidia kujenga mtindo

( f) Shughuli itekelezwe ..

3. ( a ) Ufisadi - Mandhari yataonyesha ufisadi kwa kuonyesha matukio kama vile watu kupokea na kutoa hongo , wizi wa mali ya umma .
( b) Umaskini utaonyeshwa na mandhari yanayoonyesha wahusika wakiishi kwa mfano katika makaazi hafifu kama vile nyumba za karatasi , watoto kuvaa matambara .

( c) Tofauti za kitabaka - wahusika mbalimbali watakuwa wakiishi maisha tofautitofauti kama vile wengine wakiishi maeneo ya kifahari wengine wakiishi kwa madongoporomoka , watoto wa matajiri wakisomea shule za kifahari wa maskini wakiishi shule zenye miundomsingi duni .

( d) Elimu - Kutakuwa na taasisi na shughuli za masomo katika mandhari hayo .

**II Ploti**

1 ( a) Ploti hurejelea mfuatano au mtiririko wa matukio katika hadithi .

( b) Ploti huwa na vipengele vifuatavyo

( i) Wahusika
( ii ) Mandhari
( iii) Mtindo
( iv ) Muktadha
( v) Mwanzo , kilele na hitimisho

2. ( a) Kuna aina mbili za ploti
( i) Ploti sahili - ambapo matukio hufuatana moja kwa moja
( ii ) Ploti changamano + ambapo matukio hayafuatani moja kwa moja

b) ploti huwa na umuhimu ufuatao katika hadithi...

(i) Husaidia kukuza wahusika na sifa zao. Kwa mfano katika ploti changamano mwandishi anaweza rudisha msomaji nyuma ili apate kuelewa maisha ya hapo awali ya mhusika .
(ii) Hukuza mgogoro wa hadithi na kupitia mgogoro huo ujumbe hujitokeza

(iii) Husaidia kuchochea hisia mbalimbali ambazo huimarisha ujumbe .
(iv) husaidia maamuzi ya wahusika na matokeo yake kujitokeza . Kupitia maamuzi ya wahusika ujumbe huimarika .

**Shughuli Jumuishi uk 54 .**

1. Uhusiano kati ya dhana mbalimbali za fasihi .

( a) Mandhari na ujumbe

- madhari husaidia mwandishi kukusa hisia muhimu kwa kufanikisha ujumbe . Kwa mfano mandhari magumu ya kiuchumi yatafanya msomaji apate ujumbe kuhusu unyanyasaji , n.k

( b) Mandhari na wahusika - husaidia sifa za wahusika kujitokeza .

( c) Mandhari na ploti - mandhari husaidia kukuza mgogoro ambao ni muhimu kuendeleza matukio yanayojenga ploti .

( d) Ploti na ujumbe - ploti husaidia kuimarisha na kujitokeza vizuri kwa ujumbe .

( e) mandhari na Maudhui - mandhari mbalimbali husaidia kujenga maudhui mbalimbali . Kwa mfano mandhari yakitofautina sana yanaweza jenga maudhui ya utabaka n.k..

2 ( a) Tazama maelezo ya ploti na mandhari katika uk ***

(b) Tazama aina mbalimbali za mandhari katika uk ***

(c) Zingatia umuhimu wa mandhari katika Uk*** kisha kwa kutoa mifano katika novela uliyoisoma ueleze umuhimu wa mandhari katika riwaya hiyo .

(d) Kamilisha shughuli

(e) Kwa kurejelea novela uliyosoma tambua kama ploti ni sahili au changamano .

(f) Ukizingatia umuhimu wa ploti ulioelezwa katika uk *** eleza kwa kutoa mifano umuhimu wa ploti katika novela uliyoisoma .

(g) Maelezo ya ploti yajumuishe aina ya ploti na mtiririko wa matukio .

( h ) Wasilisha uchambuzi wako wa ploti na mandhari ya novela uliyoisoma kwa wenzako .

**Nje ya darasa ( 1-2)**

Shughuli itekelezwe kwa ukamilifu .

**Shughuli ya 9 ufahamu wa kifungu cha shawishi**

1 ( a) ( i)Alikuwa akienda posta kutuma barua kwa ndugu yake anayeishi mjini .

( ii) Kumwona Boke akizungumza na mtu mwingine kwa njia ya video .

( iii) - Hutumiwa kupiga picha na kuchukua video

- Hutumiwa kuonyesha wakati na siku kwani zina saa na kalenda .

- Simu zina michezo ya burundani

- Hutumika kuhifadhi habari na data muhimu .

- Hutumiwa kama kukokotoa hesabu mbalimbali .

( iv ) Kite alikuwa na maoni hasi kuhusu simu. Kuwa simu hununuliwa kwa bei ghali na hutumia pesa nyingi kwa " credit " .

( v) Alimfafanulia jinsi simu zilivyonafuu kutegemea aina ya simu na jinsi zinavyowasilisha ujumbe kwa njia rahisi .
Pia alimpigia ndugu ya Kite Simu na akapata kuongea naye kwa urahisi .

( b) Boke aliweza kumshawishi Kite kwa sababu Kite aliamua kununua simu na kuachana na safari yake ya kuenda posta .

( c) - simu
- video
- skrini

( d) Maana ya msamiati huu wa kidigitali

( i ) Simu - kifaa kitumiwacho kuwezesha mawasiliano ya hewani kati ya watu walio mbalimbali .

*** (ii) video - kifaa / app kwenye simu kinachowezesha watu wawili au zaidi kuwasiliana huku wakionana moja kwa moja .
Pia hutumiwa kunasia picha hai na filamu.

( iii) skrini - kiwambo cha simu .

( e ) ( i) Posta - mahali ambapo barua hupokelewa na kusafirishwa

( ii ) Barua - ujumbe ulioandikwa na ambao hutumwa kwa anayelengwa kupokea kwa njia ya posta

( iii) Simu - kifaa kinachotumiwa kuwezesha mawasiliano ya hewani kati ya watu wawili walio mbalimbali
( iv ) vidude - vifaa vinavyowekwa masikioni ili kunasa sauti kutoka kwa kifaa cha kidigitali ili kumwezesha msikilizaji kusikiza bila kutatizwa na watu wengine walio karibu .

( v) Stempu - kikaratasi maalum chenye thamani fulani kinachobandikwa kwenye bahasha

kuhidhinisha usafirishaji .
( vi ) skrini - kiwambo cha simu ,mulishi .
( vii ) mawasiliano - kupashana habari kati ya watu wawili au zaidi .

( f) Sentensi zijumuishe msamiati ulio katika ( e) . Sentensi pia zizingatie kanuni za sarufi .

2. Kite anaamka asubuhi ili kuelekea posta kutuma barua kwa ndugu yake anayeishi mjini. Anapanda gari na kukutana na Boke aliyekuwa akizungumza na mtu fulani kwa njia ya skrini . Jambo hili linamshangasha . Boke anamsawishi Kite kuanza kutumia simu huku akimweleza kuwa simu si ghali kama alivyodhania . Kuwa simu hulingana na mfuko na uwezo wa mtu. Boke anashawishi Kite kununua simu na kukatiza safari ya kuenda posta kutuma barua .

( b) Wasilisha muhtasari wako kwa wenzako wautolee maoni .

**Dijitika ( a- f )**

Tekeleza shughuli hii kikamilifu .

**Nje ya darasa( 1-2** )

Tekeleza shughuli hii kikamilifu

.

**Shughuli ya 10. Kusoma kwa kina : wahusika** .

1. ( a) Ufisadi
( b) Uzembe / kukosa uzalendo
( c) Kuwa msiri
( d) Kuwa mwenye ghadhabu / mwenye hasira .

2. ( a) Uwezo wa kufanya maamuzi mema sana sana nyakati ngumu.
( b) Kufanya kazi kwa bidii
( c) Mpole - kutotumia lugha kali / asiyekasirika haraka.

( d) Kuamini uwezo wa Mungu kufanya yote/ kuomba kila wakati
( e) Kuamini uchawi
( f) Kuuliza maswali mengi .

3. ( a) wizi / udanganyifu haufai
( b) Wema hauozi / mema unayofanyia wengine hukurudia .
( c) Mvumilivu hula mbivu / ni vizuri kutokufa moyo hata wakati mambo hayaendi vizuri .
( d ) mpanda ngazi hushuka / si vyema kunyanyasa raia kwani mamlaka si ya milele

4. Vigezo vifuatavyo husaidia kutambua sifa za wahusika

( i ) Mandhari ya wahusika - kwa mfano ikiwa mhusika anaishi katika mazingira yenye uchafu jambo hili linaweza kuonyesha yeye ni mzembe

( ii ) matendo ya wahusika . Kwa mfano , mhusika anayepokea hongo ni fisadi .

( iii ) Maneno ya wahusika wengine kuhusu mhusika fulani.

( iv) Maneno na maelezo ya mwandishi .
( v) Maneno ya wahusika kujihusu yeye mwenyewe .
( vi) mambo anayopitia mhusika katika hadithi .

5. ( a) Tambua wahusika wote kwenye novela .Taja ni wepi wakuu , wadogo n.k

( b) Jadili sifa za wahusika kwa kuzingatia vigezo vya kutambua sifa za wahusika .

( c) Eleza mahusiano mbalimbali kati ya wahusika. Uhusiano huu unaweza kuwa wa kijamii , kikazi , kisiasa n.k
( d) Eleza kwa muhtasari sifa za kila mhusika .
( e) Ili kutoa mafunzo zingatia mambo yanayowapata wahusika kwa kutekeleza matendo fulani .

( f) Ukiwa na mwenzako igiza wahusika .

**Dijitika**

Ukitumia vifaa mwafaka vya kidigitali tekeleza shughuli a- c

**Nje ya darasa**

Shughuli a- c itekelezwe kikamilifu .

**Shughuli ya 11 . Kusoma kwa mapana : Matini ya Kujichagulia .**

( a ) Ujumbe wa matini haya ni kuwa watoto wana majukumu mengi katika viwango tofauti . Kuna majukumu ambayo yanawahusu wao wenyewe kama watoto binafsi , Kuna yale yanahusu marika yao , wazazi na walezi wao . Aidha watoto wana majukumu shuleni kwa jamii kubwa kwa jumla .

b) Matini haya yametumia msamiati ufuatao .

( i) majukumu ( ii) mawaidha ( iii) kibali ( iv) kijakazi ( v) wajibu ( vi) walezi .

( c) Rekodi msamiati ulioutambua .

( d) Rejelea kamusi sanifu ya kiswahili kupata maana .

( e) ( i) wajibu - lisilo bundi kutekelezwa na mtu fulani
( ii ) Faida - manufaa
( iii) Funza ** neno hili haliko kwenye matini
( iv ) Kutii - kufuata maagizo
( v) Kijakazi - mfanyikazi wa nyumbani wa kike .
( vi ) Walezi - watu ambao si wazazi wa mtoto fulani wanaomtunza na kumlea .
( vii ) Kuheshimu - kuwekea mtu adabu
( viii ) ***Maadili ( neno hili haliko kwenye matini .

( f) Sentensi zijumuishe msamiati uliopo katika ( e)
( g) ( i) amepiga mswaki - amesafisha meno kwa mswaki na dawa .
( ii) Kupiga deki - kusafisha sakafu kwa maji na ufagio
( iii) Kutia bidii - kujikaza , kutia juhudi

( h) Muhtasari uandikwe kwa aya iliyounganisha hoja zifuatazo

(i) Mtoto ni mtu aliye na umri mdogo
(ii) Mtoto anaweza kuwa wa kuzaliwa na watu fulani au wa kupangwa na walezi fulani
( iii) Watoto ana majukumu mengi katika viwango tofauti
( iv) Watoto wana majukumu yanayowahusu wao wenyewe , wazazi na walezi wao , shule , familia na jamii pana kwa jumla .
( v) Katika kiwango cha mtoto binafsi mtoto anafaa kuzingatia usafi .
( vi) Katika kiwango cha familia mtoto ana jukumu la kuwaheshimu wazazi au walezi wake , kusaidia na kazi za nyumbani na kulinda urithi na mali ya familia .

(vii ) Watoto wana jukumu la kutangamana na marika yao kwa heshima na upendo .

( viii ) Shuleni watoto wana jukumu la kutia bidii , kufuata kanuni za shule na kushiriki katika uongozi .

( ix ) Katika kiwango cha jamii pana mtoto ana jukumu la kusaidia watu wenye mahitaji maalumu.

( i) Wasilishia wenzako muhtasari wako wautolee maoni .

**Dijitika**

Shughuli za a - f zitekelezwe kikamilifu .

**Nje ya darasa**

Shughuli za a na b zimikamilishwe nyumbani .

**Shughuli ya 12 .Kusoma kwa ufasaha**

1a ) ( i ) matamshi bora ya sauti na maneno

( ii ) Kusoma kwa kasi inayofaa
(iii) Kusoma kwa sauti inayosikika
( iv) Kutumia ishara zinazofaa .

( v) Kusoma kwa kuzingatia toni na kiimbo kinachofaa .

(b) Sakura mtandaoni kupata video inayorejelewa .

(c) Tathmini ni kiasi gani usomaji huo unazingatia vipengele vilivyoorodheshwa katika ( a ) hapo juu .

3. ( a) Soma kifungu kwa kuzingatia vipengele vya usomaji bora .
( b) Shughuli itekelezwe .

**Nje ya darasa**

Tekeleza kikamilifu shughuli ya 1 na 2

**Shughuli ya 13. Kusoma kwa kina : Mbinu za lugha uk 64- 66.**

1 . Mbinu za lugha ni matumizi ya maneno au vifungu vya maneno ambavyo huipamba kazi ya fasihi na pia kusaidia kupitisha ujumbe .

2 ( a) Katika kifungu hiki mwandishi ametumia mbinu kadhaa za lugha ama za kimtindo zilizoipamba lugha yake na kuifanya ivutie na kuwasilisha ujumbe wake kama alivyokusudia.

( b) Mwandishi ametumia mbinu za lugha kama vile .

( i ) Tashbihi - kutulia sawia na maji mtunguni
- kuwa na sauti nzito kama nanga .

( ii) Nahau - ... akapiga moyo konde

( iii) Methali - Mvumilivu hula mbivu
- kikulacho ki nguoni mwako .

( iv) maswali balagha - mbona Maria ananisaliti ? Au kikulacho ki nguoni mwako ?

( v) Isitiari - alikuwa kunguru
- Maria ni simba .

( vi ) Tashihisi/ uhaishaji - mawazo yalimteka nyara .
- akachukuliwa na usingizi .

( c) Zingatia mifano iliyotolewa katika ( b) hapo juu .

( d ) ( i ) Tashibihi - imetumiwa kulinganisha hali mbili . Yaani mawazo ya Viola yalivyokuwa mazito mfano wa nanga .

( ii ) Nahau - imetumiwa kiufundi kuwasilisha maamuzi ya viola .

( iii) Isitiari - tabia ya kunguru ( woga ) inahamishwa kwa viola na tabia ya simba ( ujasiri ) inaamishwa kwa maria .
( iv) Methali - imetumiwa kusisitiza umuhimu wa uvumilivu .

( v) Maswali balagha - maswali hayo yametumiwa kutuonyesha jinsi ambavyo Viola alivyokuwa amezongwa na mawazo .

( vi) Tashihisi - mbinu hii imetumiwa kuonyesha jinsi Viola alivyozombwa na usingizi .

4. ( a) kawia ufike - Methali
( b) Yeye ni kasuku - Istiari
( c) Si hayati si mamati - msemo
( d) Mrefu kama mlingoti - tashbihi
( e) Baiskeli imeshika njia - tashihisi .

5. Zingatia mbinu za lugha zilizoorodheshwa katika **uk. 66** na majibu ya swali la **2b na 3 .**

Mifano mingine ya mbinu za lugha ni pamoja na

( i ) Taswira - maelezo yanayojenga picha za kimawazo .

( ii ) Kwelikinzani - kaulie zenye sehemu mbili zinazokinzana kwa mfano , Alicheka kwa huzuni .

( iii ) Kejeli - maelezo yanayodhihaki hali fulani.
( v) kinaya - hali inayoenda kinyume na matarajio kwa mfano mtu mzembe kuzawadiwa kazini .

Tathmini ni zipi kati ya hizi mwandishi ametumia .

( b) Zingatia umuhimu wa mbinu mbalimbali ulioelezwa katika **uk 65** katika sehemu ya kumbuka .

( c) Wasilisha kazi kwa mwenzako .

**Dijitika**

Shughuli a- c itekelezwe kikamilifu .

**Nje ya darasa**

Shughuli a- c itekelezwe kikamilifu .

**Shughuli ya 14 . Ufahamu wa Kifungu cha mjadala**

1 ( a) Habari mahususi zilizozungumziwa katika kifungu hiki ni kuhusu njia mbalimbali za kupata natija , uekezaji , njia za kuweka akiba  pamoja na nidhamu katika matumizi ya pesa .

( b) Ili awashauri wanachama kuhusiana na maswala yanayohusu  kuchuma pesa , matumizi yake na akiba .

( c) Msamiati mpya ni unaweza kujumuisha maneno yafuatayo .

( i) Ukiwa
( ii) Mtaji
(iii ) hazina
( iv) anuwai
( v) mjasiriamali
(vi) ghushi
(vii) riba
(viii)  lakabu .

( d) ( i ) Hazina - mali au pesa zilizohifadhiwa kwa matumizi ya baadaye .

( ii) riba -faida anayopata mtu kwa kuhifadhi pesa zake katika benki.

( iii) ada - malipo ambayo hutolewa na mtu ndipo apate huduma fulani.

2 ( b) habari muhimu za kifungi hiki kwa ufupi zijumuishe hoja zifuatazo

( i ) Wanachama walimwalika mtaalam wa maswala ya uchumi kwa kutaka kuelekezwa katika mambo mbalimbali.

( ii ) Mshauri katika uelekezaji wake alichukua mkondo wa mjadala .
( iii ) Wanachama walielekezwa kuhusu njia mbalimbali za kukusa mtaji na kuweka hazina .

( iv) Mshauri aliwaondolea hofu kuhusiana na kupotea kwa hazina kwa kuwaambia kuwa serikali imeweka mikakati ya kuhakikisha usalama wa mtaji.

( v) Wanachama waliondoka kwenye kikao hicho wakiwa wamefaidi pakubwa kutokana na ushauri huo.

( c) Baadhi ya wanachama walionekana kupendelea njia za zamani za kuweka hazina kama vile kuweka pesa chini ya godoro wakidai kuwa njia za kisasa kama vile benki si salama jambo ambalo lilikinzana na maoni ya mshauri .

( d) muhtasari ujumuishe hoja zilizoko katika jibu la **2 b** hapo juu. Ziunganishwe kujenga aya .

**Nje ya darasa**

Shughuli za a- d zitekelezwe kikamilifu .

**Shughuli ya 15: ufupisho**

1. ( a )aya 1: Maadili ni mwenendo na tabia njema mtu anatarajiwa kuwa nayo na jamii.

aya 2: Mavazi ni sehemu ya maadili na mtu anafaa kuvaa mavazi yenye heshima .

aya 3: Kila mtu anatarajiwa kuzingatia adabu njema anapoongea kwa kuyapima maneno yake.

aya 4: Twafaa kujiheshumu na kuwaheshimu watu wote kila wakati.

aya 5: Ni wajibu wa kila mtu kuwa na maadili .

( b) Maadili ni mienendo mizuri ya mtu. Mtu anafaa kuvaa mavazi yenye heshima yanayositiri sehemu zote za mwili. Mtu pia anafaa kupima maneno yake anapozungumza . Atumie maneno yenye heshima asiwaudhi wenzake. Heshima inafaa idumishwe kila wakati. Heshimu kila mtu bila ubaguzi. Kila mtu anawajibu wa kuhakikisha kuwa ana maadili yanayostahili .

( c) Maadili ni tabia njema mtu anatarajiwa kuwa nayo. Mtu anafaa kuvaa mavazi yenye heshima kwani mavazi humtambulisha mtu. Kuvaa mavazi yasiyosetiri uchi si tabia njema . Zingatia utumiaji wa maneno yenye heshima unapozungumza na wenzako . Yapime maneno yako ili usiwaudhi wenzako kwa sababu ya kuropokwa. Heshima inafaa idumishwe kila wakati. Wape heshima wakubwa kwa wadogo wako .Unapoketi kaa kwa njia ya heshima. Heshimu kila mtu bila ubaguzi . Heshimu vitu vya wenzako . Mali ya umma yasifujwe bali yaheshimiwe . Kila mtu

anawajibu wa kuzingatia na kuwa na maadili mema.

( d) Rejelea hatua zilizoorodheshwa katika sehemu ya **kumbuka uk 70**.

2. Shughuli ya a na b zikamilishwe .

**Nje ya darasa**

Shughuli ya 1 na 2 zikamilishwe